



**MAJI**  
Afueni kwa wakazi wa mji wa Maralal huku bwawa la Sh 1.4b la Yamo likikaribia kumalizika. UK 3



**UPATANISHO**  
Tumieni njia mbadala za kutatua mizozo kupunguza msongamano jela, asema katibu UK 6

**UTAFITI**  
Mhadhiri apata udhamini wa mamilioni ya pesa za utafiti kutoka Ujerumani

MACHI 28, 2023

# MyGov.

www.mygov.go.ke

TATHMINI YAKO YA WIKI

TOLEO No. 37/2022-2023



UK 9

## PSC kutoa ripoti kuhusu kufuata maadili na kanuni Ijumaa ijayo

**NA HABEL SHILOLI, (PSC)**

Ripoti ya mwaka wa 2021/2022 kuhusu hali ya ufuataji wa Maadili na Kanuni katika Ibara 10 na 232 ya Katiba itatolewa kwa umma Ijumaa.

Ripoti hiyo ambayo

imetayarishwa na Tume ya Utumishi wa Umma (PSC) ni kufungamana na Ibara 234 2(c) na (h) ya Katiba, inayoitaka Tume hiyo kuinua, kutathmini na kuripoti kwa Rais na Bunge, kiwango ambacho maadili na kanuni zimezin-

gatiwa kote katika utumishi wa umma.

Tume ilifanya utafiti kuhusu uzingatiaji wa mwaka wa kifedha kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2022 na ikatayarisha ripoti hiyo.

Hafu hiyo itahudhuriwa na Rais William Ruto wiki

hii katika Kenyatta International Convention Centre (KICC).

Ripoti hiyo inatoa utathmini kuhusu hatua zilizochukuliwa, mafanikio yaliyopatikana, na changamoto zinazokumba utekelezaji wa maadili na

kanuni za kitaifa na maadili na kanuni za Utumishi wa Umma.

Inapendekeza hatua za kurekebisha hali katika viwango vya ufuataji vya utumishi wa umma.

Ripoti hiyo inahusu utafiti kutoka taasisi 477 za


umma kati ya 525 ikiwa ni asilimia 91 ya kiwango kilichohusishwa.

Utafiti ulihusu kiwango ambacho taasisi za umma zilivyonyoosha Maadili na Kanuni za Kitaifa za Usi-

**ENDELEA UK 2**

## KeNIA sasa yazindua soko la mtandaoni kwa wavumbuzi

Jukwaa hilo pia linapatia biashara nafasi ya kupata ulezi, kujenga uwezo na mafunzo



**NA ROBERT OJWANG (KNA)**

Wavumbuzi vijana wa Kenya sasa watakuwa na njia tayari ya kufanya uvumbuzi wao kuwa biashara kufuatia hatua ya hivi majuzi ya Kenya National Innovation Agency (KeNIA) ya kuzindua jukwaa la dijitali kuunganisha biashara, wavumbuzi, watafiti, vituo vya tekinolojia, wafanikio na wawekezaji.

Kuzinduliwa kwa Kenya Innovation Bridge (KIB) kulifanyiwa katika

LakeHub Foundation, Kisumu. Soko hilo la dijitali litarahisishia makundi yaliyotajwa hasa kutoka Magharibi mwa Kenya kuinua uvumbuzi wao.

Jukwaa hili linapatia biashara fursa ya kupata ulezi, kujenga uwezo na mafunzo.

Chuo Kikuu cha Strathmore kilianzisha KIB kulenga kuinua kutambua wavumbuzi vijana na kuunganisha na soko mtandaoni.

**ENDELEA UK 2**

## Ushirikiano mpya wa mashirika ya ndege ya Pan-African Arline



Mashirika ya ndege ya Kenya Airways na South African Airways kuungana kubuni shirika la Pan-African Airline Group ambalo litaimarisha biashara na utalii pamoja na kutoa nauli nafuu. Ushirikiano huo unatarajiwa kukamilika kufikia 2024. PICHA: HISANI

**Takwimu za Wiki**

**1,853**

Nyumba katika kaunti ya Makueni ambazo zitapokea chakula cha msaada kutoka kwa Serikali ya kitaifa

**25,000**

Idadi ya mitandao ya WiFi ambayo serikali imemaliza kuweka katika maeneo ya umma

**64,000**

Wakazi wa mji wa Maralal, Samburu ambao watafurahia majuu safi ya kunywa kutoka bwawa la Yamo

**120M**

Kiasi cha pesa kaunti ya Trans Nzoia County imetengea akiba ya basari katika bajeti ya mwaka huu

**12,000**

Wanafunzi katika kaunti ya Taita Taveta watakuonufaika na mpango wa kupeana chakula shuleni

**20**

Ekari za ardhi ambazo shirika lililokuwa la kiserikali litatumia kuanzisha taasisi ya michezo Homa Bay



**“Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”**



## KeNIA sasa yazindua soko la mtandaoni kwa wavumbuzi

### ENDELEA KUTOKA UK 1

Mpango huo unafadhiliwa na Serikali ya Uingereza kupitia Afisi ya Maendeleo ya Kigeni ya Jumuiya ya Madola (FCDO).


Afisa Mkuu wa KeNIA Dkt. Tonny Omwansa, alisema katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Bw George Masil kwamba uunganishaji kupitia nafasi za uwekezaji, ushirikiano na ujenzi wa uwezo utaharakisha mchakato wa vijana kufanyia biashara talanta zao.

“Jukwaa la KIB linalenga kujaza pengo la ujuzi miongoni mwa wavumbuzi kupitia ujenzi wa uwezo ambao utatolewa na vituo, vyo viku na wadau wengine,” alisema Omwansa.

Wakati huo huo, alisisitiza kuwa KIB itamaliza pengo la ujumuishi kwa kuhakikisha kwamba wavumbuzi kote nchini watapata fedha, ushirikiano na wateja wa ubunifu wao.

“Tulianzisha jukwaa hili kutatua shida za watu ambao hawana washirika wanaoweza kupata soko la dijitali kuungana na washirika kadhaa kama vile serikali za kaunti,” alisema Omwansa.

Vile vile, alifichua mpango wa Shirika hilo wa kuboresha vi-



**Bw. George Masila (kushoto) akiwakilisha Dkt. Tonny Omwansa, afisa mkuu mtendaji KeNIA, Dorcas Owino (C) LakeHub Foundation, na afisa mkuu anayesimamia elimu na mafunzo ya kiufundi katika kaunti ya Kisumu Bw. John Awiti wakati wa uzinduzi wa KIB mjini Kisumu mnamo Jumatano.**

tuo vyote 260 vya kuwezesha vijana (YECs) kote nchini kuwa Vituo vya Ubunifu. Shirika hilo, kwa ushirikiano na wadau wengine litaanzisha mipango na shughuli za kujenga uwezo katika vituo hivyo ili kuvutia vijana.

“KeNIA kwa ushirikiano na Wizara ya Masuala ya Vijana, Sanaa na Michezo inataka kuhakikisha wavumbuzi kutoka maeneo yote nchini wanafahamika kupitia jukwaa hili,” alikiongeza. Mchakato huo ulian-

zishwa mwaka wa 2020 na katika hatua za mwanzo, ulivutia washiriki kutoka kaunti 20.

Shirika hilo limejitolea kupanua matumizi ya KIB kote nchini na ni kwa muktadha huu ambapo timu ilifanya uzinduzi Nakuru kwa eneo la

Rift Valley na Kisumu kwa maeneo ya Ziwa na Magharibi.

Watakuwa wakielekeza Mom-basa kwa uzinduzi wa eneo la Pwani na kumalizia Nairobi wiki zijazo.

## PSC kutoa ripoti kuhusu maadili na kanuni Ijumaa ijayo

### ENDELEA UK 1

mamizi na Maadili na Kanuni za Utumishi wa Umma, katika sehemu saba.

Sehemu hizi ni uimarishaji wa utoaji wa huduma; viwango vya juu vya maadili ya utaalumu; usimamizi mzuri, uwazi na uwajibikaji; usimamizi wa utendaji; ugavi sawa wa nafasi na rasilmali; Ushirikishi wa umma katika uundaji wa sera; na matumizi bora ya rasilmali na maendeleo endelevu.

Kiwango cha jumula cha uafikiaji kilikuwa asilimia 41.7, kikiwa kimeimarika kwa asilimia 1.7 kutoka mwaka wa kifedha uliotangulia, kumaanisha kwamba utumishi wa umma umeendelea kuimarika katika kunyoo-sha maadili na kanuni katika utoaji wa huduma.

Matokeo yanaonyesha kuwa ingawa utumishi wa umma unatoa huduma kwa raia katika maeneo mengi, kuna haja ya kuzingatiwa kikamilifu maadili na kanuni za kitaifa

za utawala katika Ibara 10; na maadili na kanuni za utumishi wa umma katika Ibara 232.

Mnamo Desemba 31 2022, PSC iliwasilisha ripoti kwa Rais na Bunge inavyohitajika kisheria.

Vile vile, Tume ilitoa ripoti ya utafiti huo kupitia semina kwa njia ya video kwa wakuu wa wafanyakazi wa taasisi zilizotathminiwa katika sekta sita za utoaji wa huduma.

Sekta hizo ni pamoja na Tume za Kikatiba na Afisi Huru (CCIOs), Wizara na Idara za Serikali (MDAs), Vyuo Vikuu vya Umma, Mashirika ya Serikali na Mashirika mengine ya serikali yaliyo na kiwango fulani cha uhuru, Tume za Kisheria na Mamlaka na Taasisi za Kiufundi na Mafunzo Anuai (TVETs).

Katika semina hizo, Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma, Balozi Anthony Muchiri alihimiza taasisi hizo kuhakikisha zimefuata maadili na kanuni za utumishi wa umma inavyoeleza Katiba.



## WIZARA YA MADINI, UCHUMI WA BAHARINI NA MASUALA YA BAHARI IDARA YA MADINI

### MWALIKO WA ZABUNI

Wizara ya Madini, Uchumi wa Baharini na Masuala ya Bahari, Idara ya Madini inawaalika wazabuni wanaostahiki kwa usambazaji/ utoaji wa bidhaa na huduma zilizoordheshwa chini kwa mwaka wa kifedha 2022-2023:

S/No	Maelezo	Nambari ya Zabuni	Hali
1	Usambazaji na Utoaji wa Vifaa vya Maabara, Vifaa vya Matumizi na Kemikali	MMBE&MA/SDM/002/2022-2023	Wazi
2	Usambazaji na Uwasilishaji wa Vifaa vya Ofisi vya Jumla na Vifaa vya Kawaida vya Watumiaji ( <b>Mkataba wa Kazi ya Mfumo</b> )	MMBE&MA/SDM/003/2022-2023	AGPO
3	Ugavi na Utoaji wa Vifaa vya ICT ( <b>Mkataba wa Kazi ya Mfumo</b> )	MMBE&MA/SDM/004/2022-2023	Wazi
4	Utoaji wa Huduma za Usafi	MMBE&MA/SDM/005/2022-2023	AGPO
5	Ugavi na Uwasilishaji wa Samani za Ofisi na Vifaa ( <b>Mkataba wa Kazi ya Mfumo</b> )	MMBE&MA/SDM/006/2022-2023	AGPO
6	Zabuni/ Usajili wa Wakala wa Usafiri wa Anga ( <b>Mkataba wa Kazi ya Mfumo</b> )	MMBE&MA/SDM/007/2022-2023	Wazi

- Seti kamili ya Hati ya Zabuni inaweza kupatikana bila malipo kwa wazabuni wanaovutiwa kwa njia ya kielektroniki kutoka kwa tovuti ya Idara ya Madini, [www.mibema.go.ke](http://www.mibema.go.ke) na tovuti ya zabuni ya Serikali ya Kenya, [www.tenders.go.ke](http://www.tenders.go.ke).
- Nyaraka za zabuni zilizokamilishwa ipasavyo zinapaswa kuambatanishwa katika bahasha tupu, iliyofungwa na iliyoandikwa jina la zabuni na nambari ya zabuni na iwekwe kwenye sanduku la zabuni lililoko orofa ya pili, Works Building, Ngong Road, Nairobi ili kufikia au kabla ya **Jumatano, Aprili 5, 2023, saa 10.00 asubuhi**. Zabuni za Kielektroniki hazitaruhusiwa.
- Zabuni zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya tarehe ya mwisho na muda uliotajwa hapo juu mbele ya wawakilishi wa Wazabuni watakoamua kuhudhuria katika Ukumbi wa Mikutano wa Orofa ya Tatu, Works Building, Barabara ya Ngong, Nairobi.
- Zabuni zilizochelewa zitakataliwa.

Katibu,  
Idara ya Madini,  
SLP 30009 - 00100,  
Nairobi, Kenya



## TUME YA UTUMISHI WA UMMU

Our Vision  
“A citizen-centric public service”

Our Mission  
“To reform and transform the public service for efficient and effective service delivery”

### NAFASI ZA KAZI KATIKA UTUMISHI WA UMMU

Tunakaribisha maombi kutoka kwa watu waliohitimu kwa nafasi zilizoonyeshwa hapa chini.



V/NO	NAFASI	WIZARA/IDARA YA WIZARA	GREDI	IDADI
17/2023	Mhajiri Mkuu wa Ardhi	Idara ya Ardhi na Mipango	CSG 4	1
18/2023	Naibu Msajili Mkuu wa Ardhi		CSG 5	2
19/2023	Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Usoroveya		CSG 5	1
20/2023	Naibu Mkurugenzi Mkuu, Uamuzi wa Ardhi na Makazi		CSG 5	2
21/2023	Naibu Mkurugenzi Mkuu, Uthamini Ardhi		CSG 5	2
22/2023	Naibu Mkurugenzi Mkuu, Mipango		CSG 5	1
23/2023	Naibu Mkurugenzi Mkuu, Usimamizi wa Ardhi		CSG 5	2

Maelezo ya nafasi na njia ya maombi yanaweza kupatikana kwenye tovuti ya Tume.

Watu wanaovutiwa na waliohitimu wanatakiwa kutuma maombi yao **MTANDAONI** kupitia tovuti ya Tume: [www.publicservice.go.ke](http://www.publicservice.go.ke) au tovuti ya kazi: [www.pscjobs.go.ke](http://www.pscjobs.go.ke) ili kufikia Tume mnamo au kabla ya tarehe **17 Aprili, 2023 (Mwisho saa 5 jioni saa za Afrika Mashariki)**

KATIBU/CEO  
TUME YA UTUMISHI WA UMMU





# Afueni kwa wakazi wa Maralal huku Bwawa la Yamo likikamilika

NA ERICK KYALO(KNA)

Familia 64,000 katika mji wa Maralal kaunti ya Samburu na vitongoji vyake hivi karibuni watapata maji safi na salama huku bwawa la Yamo lilikamilika.

Awamu ya kwanza ya Bwawa la Yamo, lililo na uwezo wa kuhifadhi lita 12 milioni za maji imekamilika na bwawa hilo linaweza kujaa katika misimu miwili ya mvua ya kawaida inayonyesha katika kaunti hiyo kila mwaka.

Mradi huo, unaotekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Maji la Kaskazini kwa gharama ya Sh1.4 bilioni unatarajiwa kuhudumia maji huo kwa wakati huu hadi mwaka wa 2038 ambapo wataalamu wanasema vyanzo vipya vya maji vitatambuliwa.

Akizungumza wakati wa ziara katika mradi huo, Katibu wa Maji na Unyunyuzaji Dkt Kiprono Rono alisema bwawa hilo linaweza kutoa lita 6 milioni kwa siku am-



**Katibu wa Maji Dkt Kiprono Paul (wa tatu kutoka kulia) akiungana na Mbunge wa Samburu West Naisula Lesuuda pamoja na maafisa wengine kutoka Wizara ya Maji na serikali ya kaunti ya Samburu wakati wa ukaguzi wa bwawa la Yamo.**

bayo yanakidhi mahitaji ya wakazi wa mji wa Maralal.

“Kazi ya ujenzi wa awamu ya kwanza ya bwawa imekamilika na awamu ya pili itahusu ujenzi wa kiwanda cha kuwekea maji dawa kitakachohitaji Sh1.5 bilioni ambazo serikali itatenga kati baajeti ijayo ili mradi huu uweze kukamilika,” alisema Kiprono.

“Pamoja na serikali ya kaunti, pia tutatambua miradi mingine ya maji katika kaunti na kupatia kipaumbele ili itengewe pesa katika bajeti miaka ijayo,” akiongeza.

Katibu huyo alihakikishia nchi kwamba serikali imeweka mipango ya kuhifadhi maji kwa kujenga mabwawa makubwa 100,

kujenga mabwawa madogo na kuchimba visima nchini.

“Kutoka kwa idara ya utabiri wa hewa, kuna ishara kwamba mvua hii haitanyesha kwa muda mrefu, na kama serikali, tumeweka hatua za kuhakikisha tumehifadhi maji kwa matumizi hasa msimu wa kiangazi,” alisema katibu.

Gavana wa Samburu Jonathan Leleliit kwa upande wake alisema changamoto kuu ya kupata maji safi ya kunywa ni kupata chanzo cha maji safi ambayo inaweza kupelekwa kwa mifereji kwa wakazi.

“Tunashukuru serikali kwa kuchagua kufanyia maadhimisho ya siku ya maji ulimwenguni hapa. Kumekuwa na changamoto za maji katika kaunti hii na tunatarajia kwamba siku hii italetika siku njema zijazo kwa watu wa Samburu kupata maji safi,” alisema Leleliit.

Mbunge wa Samburu Magharibi Naisula Lesuuda alifichua kuwa chini ya asilimia tano ya wakazi wa kaunti ya Samburu wana maji safi na salama na kwamba mengi yanapaswa kufanywa kumimarisha hali.

Lesuuda aliomba wizara ya maji kutumia muundo wa kuunganisha stima kuhakikisha kila boma limeunganishwa maji.

# Homa Bay, NGO zatia mkataba kujenga chuo cha michezo

NA SITNA OMAR(KNA)

Homa Bay hivi karibuni itakuwa mwenyeji wa soka baada ya Serikali ya Kaunti kutia saini na Shirika lisilo la kiserikali (NGO) Acakoro Football Academy kuanzisha chuo cha kukuza michezo eneo hilo.

Ushirikiano huu utafanikisha ujenzi wa chuo cha kisasa cha michezo na taasisi katika wadi ya Kanyamwa-Kosewe, kaunti ndogo ya Ndihiwa itakayonufaisha watoto wenye umri wa chini ya miaka 14. Chuo hicho cha kwanza kitajengwa katika ardhi ya ekari 20 iliyotolewa na serikali ya kaunti na kufadhiliwa na shirika hilo lisilo la kiserikali kwa gharama ya dola za Amerika 3.5 milioni.

Akizungumza baada ya kutia saini Mkataba wa Maelewano (MOU) na Meneja Mkuu wa Acakoro Bw. Lucas Mott, Gavana Gladys Wanga alisema kwamba mkataba huo unaeleza ushirikiano wa muda mrefu wa kukuza

vipawa vya eneo hilo. “Mradi huu utafungua Homa Bay kwa nafasi za kuandaa hafla kubwa za michezo. Tuko na furaha miongoni mwa kaunti 47, Acakoro, kwa usaidizi wa watu wa Austria imechagua Homa Bay kuanzisha chuo hiki,” alisema Wanga.

Acakoro iliyoanzishwa 2013 kupitia ushirikiano wa Kenyan na Austria, Acakoro imekuwa chuo kikuu cha soka Kenya kinachotoa elimu bora pamoja na shughuli za michezo.

Kitakapoanzishwa, chuo hicho, kitatoa mafunzo ya michezo na elimu kwa watoto hadi Chuo Kikuu.

“Ushirikiano huu ni wa kipekee kwa kuwa Acakoro haitajenga chuo pekee lakini pia taasisi ya masomo kusaidia watoto kusoma na pia kushiriki michezo,” alisema Wanga. Katika kituo cha mafunzo, chuo hicho kitakuwa na viwanja viwili vya soka katika awamu yake ya kwanza.



KENYA REVENUE AUTHORITY

## Public Notice

### Clean-Up of Data in Taxpayers' Register

Kenya Revenue Authority would like to notify all registered taxpayers of the on-going data clean-up exercise of taxpayers' Personal Identification Number (PIN) registration details. The exercise is aimed at ensuring the integrity of the taxpayers' register with a view to enhance service delivery to all taxpayers.

All registered taxpayers are urged to update/correct their registration details as appropriate, on iTax, including their name, phone number, physical address, email address, physical location of businesses, residency status, directorships or partnerships held e.t.c.

Taxpayers are guided to log onto itax.kra.go.ke to access their profile and follow these simple steps to update the registration details as appropriate -

1. Under the registration menu, select the option “Amend PIN details”;
2. Set the “Mode of Amendment” to Online and click the next button;
3. Check the box marked “PIN” and then select the sections you would like to update; and
4. Update the details as appropriate, attach supporting documentation where necessary and submit.

For clarification, contact the Contact Centre on Tel: 020 4 999 999, 0711 099 999 or Email: [callcentre@kra.go.ke](mailto:callcentre@kra.go.ke) or visit the nearest Tax Service Office or Huduma centre.

Commissioner for Domestic Taxes

Thank you for paying taxes to build Kenya

[www.kra.go.ke](http://www.kra.go.ke)

Disclaimer: KRA notifies taxpayers that it will not accept responsibility for payments not received, credited and validated in the relevant KRA accounts. Corruption Reporting: +254 (0726) 984 668. Email: [corruptionreporting@kra.go.ke](mailto:corruptionreporting@kra.go.ke). Short Messaging Services (SMS): Dial (\*572#) or Text to 22572. Contact Centre: +254 (020) 4 999 999, +254 (0711) 099 999, Email: [callcentre@kra.go.ke](mailto:callcentre@kra.go.ke). Complaints & Information Centre Hotlines: +254 709 017 700 / 800 Email: [ci@kra.go.ke](mailto:ci@kra.go.ke)

©KRAcare Kenya Revenue Authority Kenya Revenue Authority

Tulipe Ushuru, Tujitegeme!



KENYA INSTITUTE OF MASS COMMUNICATION  
P.O. Box 42422 - 00100 NAIROBI | Uhoro Road, Nairobi South B, off Mombasa Road  
Cell: 0708 262 895 Tel: +254 020 6997000 | Email: [info@kimc.ac.ke](mailto:info@kimc.ac.ke) | Website: [www.kimc.ac.ke](http://www.kimc.ac.ke)

## NOTISI YA TENDA

### KUMALIZA UJENZI KWENYE GHOROFA YA NNE JUU YA JENGO LILILOPO LA MAFUNZO

Kenya Institute of Mass Communication (KIMC) ambayo ni taasisi kongwe zaidi ya wastani inayotoa mafunzo ya uanahabari ambayo ilianzishwa mnamo 1961 ni shirika la kiserikali lililobuniwa kupitia Notisi No.197 ya 2011 (iliyorekebisha). Taasisi hii hutoa mafunzo kwa waliofuzu na digrii, diploma na cheti pamoja na sanaa ya kutayarisha sinema.

Taasisi inaalka maombi kutoka kwa wanakandarasi waliohitimu kumaliza ujenzi wa ghorofa ya nne ya jengo la mafunzo kama inavyoelezwa hapa chini.

S/N	JINA LA TENDA	NAMBARI YA TENDA	KUTEMBELEA ENEO LA MRADI (LAZIMA)	SIKU YA MWISHO
1	Kukamilisha ujenzi wa ghorofa ya nne katika jengo lililopo la mafunzo	KIMC/S/15/2022-2023	Aprili 4, 2023 saa 4.30 asubuhi	Aprili 18, 2023 saa 4.30 asubuhi

Wanakandarasi wanashauriwa kupakua stakabadhi yenye maelezo ya kina kutoka kwa Wavuti wa taasisi: [www.kimc.ac.ke](http://www.kimc.ac.ke) au PPIP Portal; [www.tenders.go.ke](http://www.tenders.go.ke) kuanzia Machi 28, 2023.

**Mkurugenzi**  
Kenya Institute of Mass Communication  
Uhoro Road, Nairobi South B, kando ya Mombasa Road.  
S.L.P Box 42422-00100 Nairobi  
Simu.020 6997000/0708262895

Email:[procurement@kimc.ac.ke](mailto:procurement@kimc.ac.ke)

Tunawanoa Wanahabari wa Kesho





**“Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”**



# Public participation is key to enhancing service delivery – PS

BY PENINAH KIHKA (PCO)

Devolution Principal Secretary Ms Teresia Mbaika has expressed the State Department's commitment to a people-driven and deliberately inclusive participatory process where citizen participation is at the core of policy and strategy development, selection and implementation of projects and programs.

Speaking during a Familiarization Retreat for Agencies and Departments under the purview of the National

Assembly Departmental Committee on Regional Development in Naivasha, Ms Mbaika noted that the meaningful participation of the people in decision making processes at both levels of government has gone a long way in enhancing service delivery to the citizens in the country.

The PS noted that Kenya's "Constitutional dispensation places sacred premium to public participation, consultation and cooperation", add-

ing that "the Devolved System of Government is anchored on this principle of consultation, cooperation and co-ordination".

Ms Mbaika reiterated that the State Department has been in the forefront in providing the necessary policy and administrative environment for Devolution to flourish in the country.

She also emphasized that devolution is working for Kenyans despite serious challenges that have been ex-

perienced and documented "including attempts at clawing back to centralization and re-centralizing at county headquarters.

The PS, however, stated that the State Department is alive to such challenges and has put in place various mitigation measures adding that it shall continue to "provide policy leadership, facilitation and coordination through continuous and sustained stakeholder consultation, collaboration and cooperation".

She urged the Departmental Committee on Regional Development to support the devolution sector in getting the necessary resources as the success of devolution requires huge resources for continuous civic education, structured capacity building initiatives, highly committed personnel, institutions and organizations.

The PS thanked the Departmental Committee for the existing cordial relations adding that to further enhance the relations between

the two, a Liaison Officer has been appointed so as to create a seamless link for timely consultations with the National Assembly and the Senate

Speaking during the meeting, the Chairperson of the Department Committee on Regional Development, Peter Lochakapong, said the familiarization retreat had been organized so as to create synergies between the Committee and the Agencies and Departments under its purview.

MOMBASA WATER



## MOMBASA WATER SUPPLY & SANITATION COMPANY LIMITED

MIKINDANI ST. OFF NKRUMAH RD  
P.O BOX 1100-80100  
MOMBASA.  
B/Pepe: info@mombasawater.co.ke  
www.mombasawater.co.ke

Simu: +254 041 2222700  
Faksi: +254 041 2222728  
Rununu: 0726313006  
0735655650

### NAFASI ZA KUSISIMUA ZA KAZI KATIKA SEKTA YA MAJI

NAFASI	MENEJA MKUU – HUDUMA ZA BIASHARA
IDADI YA NAFASI	1
KIWANGO CHA KAZI	2
ATARIPOTI KWA	MKURUGENZI MKUU
MFUMO WA AJIRA	KANDARASI

#### Kusudi la Kazi

Meneja Mkuu wa Huduma za Kibiashara ana jukumu la kutoa uongozi na usaidizi wa kiusimamizi bora kwa kitengo cha kibiashara, kusimamia uundaji na utekelezaji wa mikakati madhubuti ya kibiashara ambayo inahakikisha utoaji wa huduma bora, uzalishaji bora wa mapato na ukuaji wa jumla na maendeleo ya biashara ya kampuni.

NAFASI	MENEJA MKUU – UHANDISI NA MIKAKATI
IDADI YA NAFASI	1
DARAJA LA KAZI	2
ANARIPOTI KWA	MKURUGENZI MKUU
MFUMO WA AJIRA	KANDARASI

#### Kusudi la Kazi

Meneja Mkuu wa Uhandisi na Mikakati ana jukumu la kutoa uongozi bora na usaidizi wa usimamizi kwa kitengo cha kiufundi, kusimamia uundaji na utekelezaji wa mikakati madhubuti ya maji na maji machafu ambayo inahakikisha maendeleo ya kiwango cha juu cha uzalishaji wa maji safi, usambazaji na riziki. Anasimamia ubora wa maji, usambazaji bora na wa usawa na utunzaji mzuri wa mitandao yake.

#### Masharti ya Ajira

Utuzi huo utakuwa wa muda wa mkataba wa miaka 5 (mitano), unaoweza kurejeshwa na unategemea utendaji wa kuridhisha kama inavyohibitishwa na mafanikio endelevu ya vigezo vya utendaji na umahiri wa kitaaluma.

#### Utaratibu wa Maombi na Tarehe ya mwisho

Wagombea, ambao wanakidhi vigezo vilivyopo hapo juu na wana hamu ya kujunga na kundi la wafanyakazi waliohamasika, wanapaswa kuwasilisha maombi yao na CV ikiwa ni pamoja na mawasiliano ya kuaminika ya simu na barua pepe ya kibinafsi na angalau wadhamini watatu (3), ili kutufikia kabla ya Jumatatu, tarehe 17 Aprili 2023 na kutumwa kwa:

Mwenyekiti,  
Bodi ya Wakurugenzi,  
Mombasa Water Supply & Sanitation Co. Ltd,  
P.O Box 1100-80100,  
MOMBASA.

Anwani ya barua pepe: info@mombasawater.co.ke

**MOWASSCO ni mwajiri anayetoa fursa sawa ambapo wanawake na watu wenye ulemavu wanahimzwa kutuma maombi.**

#### KUMBUKA:

Tafadhali kumbuka kuwa:

- Majukumu na Majukumu Muhimu
- Elimu, Sifa za Kitaalumu na Uzoefu wa Kazi na
- Ujuzi na Umahiri umepakiwa kwenye tovuti yetu.



## TUME YA MISHAHARA NA MARUPURUPU



### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Tume ya Mishahara na Marupurupu ni Tume huru iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 230 cha Katiba ya Kenya 2010, yenye mamlaka ya kuweka na kupitia mara kwa mara Malipo na Manufaa ya Maafisa wote wa Serikali na kushauri Serikali za Kitaifa na Kaunti kuhusu Malipo na Manufaa ya wote. Maafisa wengine wa Umma. Katika kutekeleza majukumu yake, Tume haina budi kuzingatia kanuni za; uendelevu wa kifedha wa muswada wa sheria ya fidia, kuvutia na kuhifadhi ujuzi unaohitajika kwa ajili ya utoaji wa huduma, tija na utendaji, uwazi, haki na usawa.

Tume inataka kuajiri wafanyakazi wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zifuatazo zilizoachwa wazi.

1)	Afisa wa Kusimamia Rekodi	RL-6
2)	Msaidizi wa Kusimamia Maslahi ya Wafanyakazi	RL-7
3)	Msaidizi wa Kusimamia Usambazaji	RL-7
4)	Wafanyakazi Wasaidizi	RL-9

#### MCHAKATO WA MAOMBI

Watu wanaoivutwa na waliohitimu wanaombwa kuwasilisha maombi yao yanayoonyesha mshahara wao wa sasa pamoja na Wasifukazi wa Kina, Nakala ya kitambulisho cha taifa, nakala za vyeti vya elimu na taaluma na shuhuda nyinginezo. Maelezo ya nafasi hizo yapo kwenye tovuti ya Tume. Ombi la kutumwa kwa bahasha iliyofungwa iliyoandikwa "Maombi ya nafasi ya....." na kutumwa kwa barua AU kuwasilishwa kwa:

Katibu wa Tume  
Tume ya Mishahara na Marupurupu  
Williamson House Orofa ya 6  
Barabara ya 4 ya Ngong  
P.O. Box 43126 - 00100 NAIROBI

Itapokelewa mnamo au kabla ya tarehe 12 Aprili, 2023.

Tume ya Mishahara na Marupurupu ni mwajiri anayetoa fursa sawa. Watu wenye ulemavu, waliotengwa na vikundi vya wachache wanaotimiza masharti ya kazi wanahimzwa kutuma maombi. Ombi la yeyote atakayedanganya litafutiwa mbali. **Tutawasiliana na wagombea watakaoorodheshwa pekee.**

### TANGAZO LA ZABUNI

Tume inakaribisha zabuni zinazostahiki kwa yafuatayo:-

Na	Namba ya Marejeleo	Maelezo ya Zabuni	Uhitimu	Dhamaba	Kufunga
1.	SRC/OT/55/2022- 2023	UTOAJI BIMA YA MATIBABU KWA WANACHAMA WA TUME NA WAFANYAKAZI WA TUME YA MISHAHARA NA MARUPURUPU (SRC).	WAZI	100,000	Aprili 13, 2023
2.	SRC/OT/56/2022-2023	UTOAJI WA HUDUMA ZA TIKETI ZA NDEGE	AGPO	N/A	Aprili 13, 2023

Waombaji wanaoivutwa wanaweza kupata hati ya zabuni kutoka kwa tovuti ya SRC [www.src.go.ke](http://www.src.go.ke) au Tovuti ya Taarifa ya Ununuzi wa Umma ([www.tenders.go.ke](http://www.tenders.go.ke)) bila gharama yoyote.

Hati kamili zitawekwa kwenye Sanduku la Zabuni lililo kwenye lango la Ofisi za Tume ya Mishahara na Marupurupu, Orofa ya 6, Williamson House, Nairobi, au kutumwa kwa

Katibu wa Tume  
Tume ya Mishahara na Marupurupu  
P.O. Box 43126-00100  
NAIROBI

Ili kupokelewa kabla au kabla ya tarehe ya kufungwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo juu.

Zabuni itafunguliwa mara moja katika chumba cha mikutano cha SRC kwenye ghorofa ya 6, Williamson House, mbele ya wazabuni wanaotaka kuhudhuria.

#### KATIBU WA TUME

<https://www.src.go.ke/>

Salaries and Remuneration  
Commission

@SRCKE

@srckeny



Funika mdomo unapopiga chafya



Nawa mikono na sabuni/ Sanitaiza



Jitenge na walio na virusi



Usiguse macho, uya au mdomo na mikono michafu



Pika nyama na mayai ziive. Usile chakula kibichi



Hakikisha maeneo yote ni safi



UZUIAJI

MACHI 28, 2023

MATANGAZO | 5



## NATIONAL OPEN TENDER NOTICE

The National Construction Authority (NCA) is a State Corporation established under the National Construction Authority Act 2011, with the responsibility to oversee the construction industry and coordinate its development. The Authority invites sealed bids from eligible candidates for the following tenders;

No	Tender	Description of Tender	Eligibility	Closing
1.	NCA/T/017/2022-2023	Supply of 4x4 Double Cab Pickups and Sport Utility Vehicle	Open	5th April, 2023

Tender document with detailed information and instruction may be viewed and downloaded from the Authority's website; [www.nca.go.ke](http://www.nca.go.ke) and the Public Procurement Information portal, [www.tenders.go.ke](http://www.tenders.go.ke) free of charge.

Manager Supply Chain

FOR: EXECUTIVE DIRECTOR

[@ncakenya](https://twitter.com/ncakenya) [National Construction Authority](https://www.facebook.com/ncakenya) [info@nca.go.ke](mailto:info@nca.go.ke) [+254-709 126 102/172/173](tel:+254709126102172173)



REPUBLIC OF KENYA

## MWALIKO WA TENDA



Kenya Power

Kenya Power inaataka wanaotaka kushiriki tenda zifuatazo kutuma maombi:-

NO.	NAMBARI YA TENDA	MAELEZO YA BIDHAA	TAREHE YA KUANZA KWA TENDA	TAREHE YA MWISHO
1	KP1/9A.3/OT/32/22-23	Kununua mseto wa vipuri na vifaa vya karakara za Viwanda vya Umeme	Jumanne 28.03.2023	Jumanne 25.04.2023 Saa 4.00 asubuhi.
2	KP1/9A.2/OT/061/ICT/22-23	Utoaji wa huduma za kutuza leseni ya kila mwaka na IP PBX	Jumatano 29.03.2023	Jumatano 12.04.2023 Saa 4.00 asubuhi.
3	KP1/9A.3/OT/030/22-23	Ununuzi wa injini za mwendu wa kadri za 2x1MW kutumika katika kituo cha umeme cha Wajir	Ijumaa 31.03.2023	Jumanne 25.04.2023 Saa 4.00 asubuhi.

Stakabadhi za tenda za kuelezea kwa kina mahitaji kamili ya tenda hizo zinaweza kupatikana kutoka kwa wavuti wa Kenya Power ([www.kplc.co.ke](http://www.kplc.co.ke)) kuanzia tarehe zilizotajwa hapo juu.

MENEJA MSIMAMIZI, UNUNUZI NA UCHUKUZI

[www.kplc.co.ke](http://www.kplc.co.ke)

DIAL \*977# | Access Kenya Power services fast and easy

[www.kplc.co.ke](http://www.kplc.co.ke) @Customercare.kplc.co.ke Kenya Power @KenyaPower 97771 0703-070 707, 0732-170 170



## MINISTRY OF INVESTMENTS, TRADE AND INDUSTRY

### STAKEHOLDERS CONSULTATION FORUMS

#### PUBLIC PARTICIPATION FORUMS ON THE EXPORTS AND INVESTMENTS PROMOTION LEVY

The Ministry is intending to introduce an export and investment promotion levy to support local manufacturing, spur investments and increase exports.

In accordance with Article 10(2)(a) of the Constitution, that highlights National Values and Principles of Governance including participation of the people, the Ministry through this Notice, hereby invites members of Public and Stakeholders to give their comments during these consultative forums in the following areas and venues as indicated :-

TEAM	DATE	REGION	COUNTIES COVERED	VENUE	TIME
1.	4 <sup>th</sup> April, 2023	Machakos	Nairobi, Machakos, Kajiado, Makeni, Kitui and Kiambu Counties	Machakos University	10:00 a.m.
	6 <sup>th</sup> April, 2023	Garissa	Garissa, Mandera and Wajir Counties	Garissa University	10:00 a.m.
2.	4 <sup>th</sup> April, 2023	Mombasa	Mombasa, Taita Taveta, Kwale	Technical University of Mombasa	10:00 a.m.
	6 <sup>th</sup> April 2023	Malindi	Kilifi, Lamu and Tana River Counties	Pwani University College	10.00 a.m.
3.	4 <sup>th</sup> April, 2023	Meru	Embu, Meru, Tharaka Nithi, Marsabit and Isiolo Counties	Meru University	10.00 a.m.
	6 <sup>th</sup> April, 2023	Nyeri	Nyeri, Kirinyaga, Murang'a, Nyandarua and Laikipia Counties	Dedan Kimathi University	10.00 a.m.
4.	4 <sup>th</sup> April, 2023	Kisii	Kisii, Nyamira and Migori Counties	Kisii National Polytechnic	10:00 a.m.
	6 <sup>th</sup> April, 2023	Kisumu	Kisumu, Siaya and Homa Bay Counties	Kisumu National Polytechnic	10:00 a.m.
5.	4 <sup>th</sup> April, 2023	Kakamega	Bungoma, Kakamega, Busia and Vihiga Counties	Masinde Muliro University	10:00 a.m.
	6 <sup>th</sup> April 2023	Kitale	West Pokot, Turkana, Trans Nzoia,	Kitale Polytechnic	10.00 a.m.
6.	4 <sup>th</sup> April, 2023	Nakuru	Nakuru, Baringo, Samburu, Narok, Kericho and Bomet Counties	Kenya Industrial training Institute (KITI)	10:00 a.m.
	6 <sup>th</sup> April, 2023	Eldoret	Uasin Gishu, Nandi and Elgeyo Marakwet Counties	Eldoret National Polytechnic	10.00 a.m.

Members of the Public and Stakeholders may also send their written memoranda through the following email address [ps@industrialization.go.ke](mailto:ps@industrialization.go.ke) or through **P.O. Box 30418-00100 Nairobi** on or before **14<sup>th</sup> April 2023**. You may also visit our website for more information on [www.industrialization.go.ke](http://www.industrialization.go.ke)



REPUBLIC OF KENYA

## THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL



### TENDER NOTICE

1.0 The Kenya National Examinations Council (KNEC) is a State Corporation established in 1980 under an Act of Parliament, namely the Kenya National Examinations Council Act Chapter 225A of (1980). The Act was repealed in 2012 and replaced with the Kenya National Examinations Council Act No. 29 of 2012. The Council is mandated to conduct national assessments and examinations at both basic and tertiary levels and certify learners.

2.0 KNEC invites sealed bids from eligible bidders for the Tenders below:

S/No.	TENDER NUMBER	TENDER TITLE	TARGET GROUP
2.1	KNEC/ONT/2022-2023/17	Servicing, Repair and Maintenance of Generators, Water Pumps and Air Compressors	Open
2.2	KNEC/ONT/2022-2023/18	Servicing, Repair and Maintenance of Electric Fences and Pedestrian Turnstile Barriers	Open
2.3	KNEC/ONT/2022-2023/19	Servicing, Repair and Maintenance of Lifts	Open
2.4	KNEC/ONT/2022-2023/20	Servicing, Repair and Maintenance of Safes, Bulk Filers, Security Doors and Office Furniture on a frame work contract.	Open
2.5	KNEC/ONT/2022-2023/21	Servicing, Repair and Maintenance of Fire Suppression Systems	Open
2.6	KNEC/ONT/2022-2023/22	Provision of Office Cleaning and Fumigation Services	Women
2.7	KNEC/ONT/2022-2023/23	Provision of Security Guarding Services	Open
2.8	KNEC/ONT/2022-2023/24	Disposal of Waste Paper and related materials	Open
2.9	KNEC/ONT/2022-2023/25	Supply and Delivery of Bulk Printing Paper and Related Consumables	Open
2.10	KNEC/ONT/2022-2023/26	Supply, Installation, Testing and Commissioning of Specialized Printing Equipment	Open
2.11	KNEC/EOI/2022-2023/02	Provision of Peer Review Services	Open
2.12	KNEC/EOI/2022-2023/03	Provision of Occupational Health and Safety Services	Open

3.0 Interested eligible Bidders may obtain tender documents from the following websites: [www.knec.ac.ke](http://www.knec.ac.ke) or [www.supplier.treasury.go.ke](http://www.supplier.treasury.go.ke) or [www.tender.go.ke](http://www.tender.go.ke)

4.0 The closing date for submission is on **13<sup>th</sup> April, 2023 at 10.00 a.m.** Application is open to all interested bidders.

CHIEF EXECUTIVE OFFICER





**“Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”**



# Tumieni njia mbadala kutatua mizozo kupunguza msongamano katika jela



**Katibu wa Huduma za Kurekebisha Tabia Bi Mary Muthoni Muriuki apanda miti wakati wa siku ya kimataifa ya misitu katika msitu wa Marmanet, kaunti ya Laikipia.**

NA ANTONY MWANGI (KNA)

**K**atibu wa Idara ya Huduma za Urekebisha Tabia Bi Mary Muthoni Muriuki ameshauri wakazi wa kaunti ya Laikipia ku-

kumbatia Njia Mbadala za Kutatua Mizozo (ADR) badala ya kupeleka kesi kortini.

Akizungumza akiwa kaunti ndogo ya Laikipia Magharibi katika hafla ya

kupanda miti kuadhimisha siku ya Kimataifa ya Misitu katika msitu wa Marmanet, Bi Muriuki alisema ADR ni ajenda inayopaswa kukumbatiwa na wote.

Zoezi hilo la kupanda miti

lilifanywa na wafungwa 166 walioachiliwa wiki jana na Idara ya Magereza.

Miti iliyopandwa itafuatiliwa na kutunzwa na wafungwa waliopatiwa kifungo cha nje kwa ushirikiano na Idara ya Misitu Kenya.

Hatua hii, alisema, inafungamana na agizo la rais la kupunguza msongamano katika magereza nchini. Agizo hilo lilitolewa na Rais katika hafla ya kufunzu maafisa wa magereza katika chuo cha magereza cha Ruiru.

Katibu alihimiza Mahakama kuwahamasisha machifu na viongozi wengine wa mashinani kukumbatia njia mbadala ya kutatua mizozo kabla ya kwenda kortini, hasa kwa makossa madogo na ya kijamii.

Alisema kwamba kwa wale ambao tayari wako jela, serikali imeanzisha mpango wa Kutumia Jamii na akahimiza maafisa wa probesheni kufika kortini na kuchunguza kesi ndogo na kuhakikikisha wameachiliwa huru.

Aliongeza kuwa wale ambao tayari wako jela, serikali imeanza mpango wa kutumikia jamii na akahimiza maafisa wa probesheni kwenda kortini na kuchun-

guza kesi ndogo ndogo ili waachiliwe huru.

“Kabla ya mtu mwenye makosa madogo apelekwe kortini, ni vizuri tujaribu kukumbatia mchakato mbadala wa kutatua kesi katika kiwango cha kijiji.

“Kwa wale walio jela leo, tumeanza mpango wa kutumia jamaa ambapo maafisa wa probesheni wataenda kortini, wabadilisha hukumu hizo na kuhakikisha wafungwa wa makossa madogo wanaachiliwa huru na kuwekwa chini ya CSO kufanya kazi bila malipo kama upanzi wa miti,” alisema katibu.

Alisema kwamba serikali huwa inatengea kila mfungwa Sh275 kwa siku na akaongeza kuwa serikali inapata hasara kubwa kuwatumia wafungwa.

Alisema pesa hizo zinaweza kutumiwa kwa miradi ya maendeleo. “Uchumi wetu unategemea pakubwa misitu asili. Nina-taka kuomba viongozi wetu na wakazi kuhakikisha tumepanda miti katika nchi yetu kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Katibu aliongoza upanzi wa miti miche zaidi ya 100,000 katika msitu wa Marmanet, idadi aliyosema itaendelea kuongezwa kupitia washirika.

## TBK yanasa mashini mbovu za upimaji chai

NA MWANDISHI WA MYGOV

Bodi ya Chai ya Kenya (TBK) kwa ushirikiano na Idara ya Vipimo imenasa mashini mbovu za kupima chai kwenye msako wa ghafla wa vituo kadhaa vya kununua chai Kaunti ya Bomet.

Hii inafuatia malalamishi ya wakulima wa mashamba madogo ya Chai waliolaumu wasimamizi wa kampuni za kampuni za chai kwa kuwapa kwa kubadilisha vipimo kila mara wanapopeleka chai katika vituo vya ununuzi vya Shirika la Maendeleo ya Chai la Kenya (KTDA).

Akizungumza na wanahabari katika kituo cha kununua chai cha Rorok, meneja wa Uzingatiaji na Ufuatiliaji wa Bodi ya Chai ya Kenya Samuel Njane alisema ziara hiyo wa ghafla katika viwanda kadhaa za chai ilitokana na malalamishi ya wakulima wa chai.



### TENDER NOTICE

The Kenya Civil Aviation Authority invites sealed bids from interested and eligible firms for the following National Open Tenders.

NO	TENDER NUMBER	TITLE OF TENDER	PRE-BID/ SITE SURVEY DATE	ELIGIBILITY	CLOSING DATE
1.	KCAA/059/2022-2023	Proposed Construction of Air Traffic Control Tower At Kisumu International Airport	Thursday, 13 <sup>th</sup> April, 2023 at 11am to 2.00pm at Kisumu International Airport Control Tower	Citizen	Tuesday, 25 <sup>th</sup> April, 2023 at 11am

For more information on the various tenders, bidders may view and download the bidding documents from KCAA website: [www.kcaa.or.ke](http://www.kcaa.or.ke) or Public Procurement Information Portal, [www.tenders.go.ke](http://www.tenders.go.ke) and immediately forward their particulars for records and for the purposes of receiving any further tender clarifications and/or addendums to [procurement@kcaa.or.ke](mailto:procurement@kcaa.or.ke)

Completed tender documents are to be enclosed in plain sealed envelopes marked with tender reference number and be deposited in the Tender Box at the Ground Floor, Kenya Civil Aviation Authority, Aviation House, Jomo Kenyatta International Airport, or be addressed to:

**The Director General,  
Kenya Civil Aviation Authority,  
P.O Box 30163-00100, Nairobi**

So as to be received on or before **Tuesday, 25<sup>th</sup> April, 2023 at 11:00 am.**

The tenders will be opened immediately thereafter in the presence of the Candidates or their representatives who choose to attend at KCAA Auditorium.

**Manager Procurement  
FOR: DIRECTOR GENERAL**



## Kenya National Innovation Agency

### INVITATION TO OPEN NATIONAL TENDER

The Kenya National Innovation Agency (KeNIA) is a State Corporation established under the STI Act, No. 28 of 2013 under the Ministry of Education with the mandate to develop and manage the National Innovation System.

KeNIA invites sealed tenders for the following:



S/ No	Tender No	Description	Category	Closing Date
1.	KENIA/ONT/01/2022-2023	Provision Of Fuel, Oil and Lubricants Using Fuel Card System for Kenya National Innovation Agency Motor Vehicles	All	5 <sup>th</sup> April, 2023

Interested and eligible bidders may view the tender documents from the KeNIA website ([www.innovationagency.go.ke](http://www.innovationagency.go.ke)) or Public Procurement Information portal ([www.tenders.go.ke](http://www.tenders.go.ke)) or at KeNIA Supply Chain Management Office at NACOSTI Building, ground floor, off waiyaki way for detailed descriptions. Interested and eligible bidders should download the tender document from the above websites free of charge and immediately email their names and contact details to: [procurement@innovationagency.go.ke](mailto:procurement@innovationagency.go.ke) for records and communication of any tender clarifications or addenda.

